# Jinsi biashara zinavyofanyika Vingunguti-2

Mariam Mbwana, Mwananchi
mmbwana@mwananchi.co.tz



**NUKUU**

**"Hapa mteja anaweza kupata nyama kwa bei tofauti, kuna nyama huuzwa Sh4,000 kwa kilo, pia kuna zinazouzwa kwa mafungu ambazo hupatikana nje ya machinjio na kila fungu hupatikana kwa Sh2,000 hadi Sh1,000."**

**John Lauren**

**RIPOTI MAALUMU**

**Dar es Salaam.** Katika Machinjio ya Vingunguti, Dar es Salaam hakitupwi kitu. Hilo ni jibu, si swali kama utafika katika machinjio hayo yaliyojaa kila aina ya raha na usumbufu kwa baadhi ya watu, hasa wageni wa eneo hilo.

Si ajabu kukuta kwato za ng'ombe zikigombewa, achililia mbali ngozi na supu ambazo bei yake ni kati ya Sh500 hadi 1,500.

Akizungumza namna wafanyabiashara hao wanavyotumia fursa ya vitu vya mifugo baada ya kuchinjwa, kiongozi wa wafanyabiashara wa machinjio hayo, Joel Meshack anasema zipo taarifa kuwa sehemu za siri za ng'ombe zinachukuliwa na Wachina kwa ajili ya kutengenezea nyuzi za kushonea binadamu kipindi cha operesheni.

"Unajua hivi vitu wenyewe hawapendi kuvieleza, lakini kuna taarifa baada ya ng'ombe kuchinjwa zinachukuliwa sehemu za siri na Wachina wanaenda kutengenezea nyuzi za kushonea kipindi cha operesheni. Pia wengine husema baada ya kukaushwa husagwa na kupewa wanawake wanaonyonyesha ili watoe maziwa mengi," alisema Meshack.

Kwa upande wa ngozi, Lameck anasema zinasafirishwa nje ya nchi na kuna mataifa wanatumia kama chakula. Kwato pia hutumika kutengenezea gundi.

"Kwenye ng'ombe kuna mambo mengi, Waafrika hatuna utaalamu wa kutosha, hivyo kazi yetu ni kuzalisha malighafi zinazotokana na ng'ombe lakini matumizi wanayajua wahusika," alisisitiza.

Katika Machinjio ya Vingunguti kumekuwa na mkusanyiko mkubwa wa watu, purukushani za hapa na pale hasa asubuhi na usiku, muda ambao wanyama huchinjwa na muda huo binashara ndio hufanyika kwa wingi ukilinganisha na mchana au jioni.

Ukifika eneo hilo salamu ya kwanza kwa vijana waliopanga bidhaa zao kwenye meza pembeni mwa barabara ya Vingunguti ni "Karibu mteja fungu moja ni Sh 2,000."

Hali hiyo ilinifanya kusogea karibu kutaka kufahamu undani wa bidhaa hizo.

Mmoja kati ya wafanyabiashara wa nyama, John Lauren anasema wanyama wanaochinjwa kwa wingi ni n'gombe, mbuzi pamoja na kondoo. "Kwa siku ng'ombe, mbuzi na kondoo wanaochinjwa hapa ni takribani 500 na huanza kuchinjwa nyakati za usiku," anasema Lauren.

Kwa sasa katika maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam nyama kilo moja huuzwa kati ya Sh6,500 hadi Sh 8,000, lakini katika machinjio hayo huuzwa Sh5,000 kwa kilo.

Pia kuna nyama zinazouzwa kwa mafungu ambazo huuzwa Sh2,000 kwa fungu moja na ikifika jioni unaweza kupata hadi kwa Sh1,000.

"Hapa mteja anaweza kupata nyama kwa bei tofauti, kuna nyama huuzwa Sh4,000 kwa kilo, pia kuna zinazouzwa kwa mafungu ambazo hupatikana nje ya machinjio na kila fungu hupatikana kwa Sh2,000 hadi Sh1,000 ifikapo mida ya jioni," anasema Lauren.

Anasema unafuu wa bei hautokani na madai kuwa huokota masalia na kwenda kuuzia watu, bali unatokana na kuwa wapo kiwandani.

Mmoja ya wateja katika eneo hilo ambaye hakutaka kutaja jina alisema nyama pamoja na bidhaa nyingine zinazopatikana Machinjio ya Vingunguti zinauzwa kwa bei nafuu ukilinganisha na bei unaponunua mtaani.

"Napenda kuja kufanya manunuzi yangu ya mboga hapa kwa sababu ni rahisi ukilinganisha na kule katika mabucha yetu ambapo kilo moja ya nyama ni Sh8,000," anasema.

Tofauti na biashara ya nyama kumekuwa na wafanyabiashara wanaoendesha maisha yao kupitia uuzaji wa viungo vya ndani ya ng'ombe kama maini, bandama, mapupu, utumbo, kongoro, mkia, koromeo, ulimi pamoja na kichwa.

Kwenye maini na utumbo nako unachagua na kulipia Sh2,000.

Kwa upande wa kongoro hupatikana pia kwa Sh2,000 hadi 2,500 kutegemea na namna biashara ilivyo kwa siku husika.

Bandama, mapupu, mkia, koromeo, ulimi pamoja na kichwa huuzwa kwa maelewano kati ya muuzaji na mnunuaji.

Wateja wao wakubwa ni wafanyabiashara wa chakula wanaoonekana pembeni wakiwa katika harakati za kutengeneza mishikaki na kuchemsha supu.

Mishikaki na supu huambatana na mihogo, chapati na maandazi ambayo hukaangwa zaidi na wanawake.

Mbali na hao, pia wapo wanaopata riziki kupitia uchomaji wa ubongo pamoja na korodani ambazo kwa Sh500 unapata.

*Itaendelea kesho*

**Sh2,000**

**Bei ya fungu la nyama machinjio ya Vingunguti.**

**Sh500**

**Bei ya korodani zilizochomwa pamoja na ubongo.**

Scanned with CamScanner

# Wavuvi wakimbia Bwawa la Mtera

**Na Sifa Lubasi,Dodoma**

WAVUVI katika na bwawa la Mtera Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, wamelazimika kuhamia mikoa mingine yenye mabwawa kutokana na uhaba mkubwa wa upatikanaji wa samaki.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari kwenye maeneo ya makambi ya wavuvi ya Mapera Mengi, Chadumbwi na Migoli walisema kuwa pamoja na kuwepo kwa maji mengi lakini bado upatikanaji wa samaki umekuwa ni mgumu.

Mmoja wa wavuvi hao, Jacob Mwalukali alisema kutokana na hali hiyo wakazi walio wengi wanaojishughulisha na uvuvi wameathirika kiuchumi hivyo imewalazimu kufuata samaki kwenye maeneo mengine kama mikoa ya Singida, Kilimanjaro, Arusha na wilayani Bahi.

Simon Lukui kutoka kambi ya Migoli alisema kuadimika kwa samaki katika bwawa hilo, shughuli mbalimbali za kimaisha zimekuwa ni ngumu ikiwemo suala la kuwalipia watoto ada na hata kwenye kupata matibabu.

"Maji yamejaa kwenye bwawa letu lakini cha kushangaza samaki hakuna kabisa, hawa mnaowaona wanatoka kwenye bwawa lililopo huko Bahi Nagulo na wengine wanatoka mikoa ya Singida, Arusha na Kilimanjaro," alisema Lukui.

Alisema pia kuna uvuvi haramu katika bwawa hilo na kusababisha kuadimika kwa samaki hao, hali ambayo imechangia wavuvi na wachuuzi kwenda kwenye maeneo mengine yenye mabwawa

Kwa upande wake Mshauri Mkuu wa Umoja wa Makanisa ya Kipentekoste Mtera, Askofu Mstaafu Aswelle Mwandamo aliwataka wakazi wanaoishi kwenye makambi yaliyopo kando kando ya bwawa hilo la samaki la Mtera kujiwekea ulinzi wao wenyewe ili waweze kuwabaini wanaotumia uvuvi haramu badala ya kuliacha suala hilo mikononi mwa serikali.

Kiongozi huyo wa kiroho aliwataka wakazi hao kushirikiana na serikali katika masuala mbalimbali ikiwemo, elimu jinsi ya kulilinda bwawa hilo na namna ya kujiepusha na matumizi ya uvuvi haramu kwa waumini wao.

Alisema hiyo ni pamoja na wanaoharibu mazingira ya bwawa hilo ambalo limekuwa likiwawezesha kujikwamua kiuchumi na pia ukizingatia kuwa chanzo kikuu cha kitaifa katika uzalishaji wa nishati ya umeme.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Unjilisti na Ualimu wa umoja huo wa makanisa ya kipentekost Mtera Askofu mstaafu wa Kanisa la EAGT Jackson Madelemo akizungumza na wakazi wa Mtera aliwaomba waendelee kuombea mahitaji mbalimbali muhimu kwa ajili ya taifa na eneo zima la Mtera.



## Jokate akabidhi ofisi kwa Nickson

Scanned with CamScanner